Pasaka na Meza Ya Bwana Sehemu Ya 1
(Passover & The Lord's Supper Part 1)

Na
Ellis P. Forsman

Pasaka Na Meza ya Bwana
Sehemu ya 1

Na
Ellis Forsman

Desemba 16, 2016

Pasaka Na meza ya Bwana – Part 1
Utangulizi: Luke 22:1-20

Miaka kadhaa iliyopita, nilifanya kazi na mwajiriwa mwenzangu ambaye alikuwa Myahudi wa kiorthodox. Nilitaka kujua baadhi ya desturi ya Wayahudi na maadhimisho ya sherehe zao, hivyo nilimuuliza maswali kadha wa kadha kuhusu pasaka. Maelezo aliyonipa yalinipa mwanga.

Miaka kadhaa baadaye, mimi na mke wangu tulikutana na mwanamke ambaye pia alikuwa Myahudi wa Kiorthodox; taarifa alizotupa zilifanana na zile tayari tulikuwa tumejifunza na Yule Myahudi wa kwanza. Mama huyu baadaye alifanyika muumini wa kanisa la Kristo. Baadaye kwa upande wangu niliendelea kusoma kuhusu Pasaka na kujazwa katika elimu yangu. Sehemu ya 1 ya makala hii ni matokeo ya utafiti wangu na ina zaidi Sehemu ya utafiti kuhusu Meza ya Bwana na maadhimisho ya Pasaka katika akili.

Kama wengi wenu mnavyojua, wakati Bwana alipoanzisha kile kinachoitwa "Meza ya Bwana" alikuwa akila chakula pamoja na wanafunzi wake katika kile tunachoita Pasaka. Wayahudi hutambua chakula hiki kama "sikukuu ya mkate usiochachwa", "Msimu wa Uhuru wetu", na "kupita juu". Neno la mwisho linalotumika kwa kawaida, hata miongoni mwa Wayahudi. kielelezo ni jinsi gani katika sura ya 12 ya Kutoka, wakati malaika wa kifo alipouwa wazaliwa wa kwanza wa kila nyumba ambao hawakupaka damu ya mwana kondoo katika miimo ya milango yao.

Unaweza kusoma ripoti kamili ya tukio hili katika sura ya 12 ya kitabu cha Kutoka.

Mungu aliwaamuru Wayahudi kuchunguza siku hii katika Mwanzo.12:14 kama ifuatavyo: "*Na siku hii itakuwa kwenu kwa ajili ya kumbukumbu, nanyi mtaishika kuwa sikukuu kwa Bwana katika vizazi vyenu; Nanyi mtaishika kuwa sikukuu kwa amri ya milele.*"

Neno "milele" maana yake "mpaka hatua ya kutoweka" katika Kiyunani. Haina maana "yasiyoisha" kama mawazo ya kawaida. Hatua ya kutoweka kwa Pasaka ilitokea wakati Yesu alipokufa msalabani. Basi, Wayahudi waliendelea kutunza sikukuu hii kila mwaka kwa vizazi vyote tangu wakati wa Musa mpaka msalaba wa Yesu.

Mkuu wa familia ya Kiyahudi alikuwa akihakikisha kuwa ana adhimisha sherehe hii kila mwaka jioni ya Siku ya 14 ya mwezi wa Nisan (inaweza kuwa Machi au Aprili, kulingana na mwezi katika mwaka wowote).

Miezi ya wayahudi huanza kwa mbalamwezi uliyo kamilika , hivyo ilikuwa rahisi kwa Wayahudi wakati wa kuhesabu siku ambayo Pasaka ingetokea. Pasaka ingeweza kutokea siku yoyote ya juma. Bila kujali ni siku ipi ya wiki ambayo Pasaka imetokea, ilikuwa inajulikana kama Sabato Kuu na Jumamosi ya kwanza baada ya Pasaka ilikuwa inajulikana kama Sabato ya kawaida.

Tunajua kuwa kanisa ilianzishwa Siku ya Pentekoste ambayo mara zote ni siku ya kwanza ya juma. Wayahudi wanachukulia sikukuu ya Pentekoste kama Sikukuu ya Majuma saba mara 7 ambayo ni siku 49 na kuongezea siku moja baada ya Sabato ya kawaida ambayo ilifuatiwa na Sabato kuu (Pasaka), hivyo siku 50 (penta).

Kwa mfano, kama wakati wa mwezi wa Kiyahudi wa mwezi Nisani wakati viongozi wa Wayahudi walipo adhimisha Pasaka, mwezi kamili ilitokea Jumatano ilikuwa inaitwa Sabato kuu; Jumamosi ya kwanza baada ya Pasaka ilikuwa inaitwa Sabato ya kawaida. Siku ya Pentekoste inge hesabiwa siku 50 (majuma 7 na kuongeza siku moja) kutoka Sabato ya kawaida. Ilikuwa daima hutokea siku ya kwanza ya juma ambayo ni Jumapili.

Sherehe ya Pasaka

Mgawanyiko wa Wayahudi

Jinsi kulivyo na mgawanyiko katika ulimwengu wa Kikristo (wabaptist, kusanyiko la Mungu, Katoliki, Methodist, nk), ndivyo ilivyo kati ya Wayahudi. Kuna Myahudi wa Kiorthodox, Myahudi aliye hasi, Myahudi aliye rejeshwa, Myahudi aliye huru kwa kufikiria, na Myahudi asiye juwa kuwa Mungu yupo.

Kulikuwa na migawanyiko kuu mbili ya Wayahudi wakati wa Kristo: Mafarisayo na Masadukayo. Masadukayo walikuwa sawa na Myahudi wa leo kwa sababu hawakuamini katika ufufuo wa wafu. Myahudi asiye amini alikuwa ni Myahudi wa kiutaifa tu, hawaamini katika uwepo wa Mungu.

Haya madhehebu tofauti tofauti leo wanatofautiana katika imani zao na vitendo; maadhimisho ya Pasaka hakuna ubaguzi. Myahudi wa Kiorthodox leo anatambua Pasaka kwa karibu zaidi na madhubuti na ile ya wakati wa Agano Jipya, lakini hata wao wameteleza katika maadhimisho yao. Tutaangalia hili baadaye kidogo, hata hivyo, tutaitaji kuangalia Desturi ya Wayahudi ya Pasaka kama ilivyotokea wakati wa Kristo.

Maandalizi ya Pasaka

Kabla ya Pasaka ya Kiyahudi mkuu wa kaya huanza kusafisha nyumba toka juu mpaka chini kutowa chachu yote. Chachu kwa Myahudi inawakilisha dhambi. Kila nook na mwanya inapata angalizo. Hakuna uchafu ambao ungebaki na jiko, birika, na nguo ni lazima zikaguliwe kwa makini; hakuna nusu ya chachu iliyopaswa kuachwa popote. Zulia walikuwa wanatoa nje na kukung'utwa, mifuko ya nguo zote walikuwa wanatoa nje na kuzigeuza ili kukung'utwa kwa makini, kama Ukuta ulikuwa na pambo, lilikuwa lina chanwa na ukuta kusafishwa na kupakwa rangi upya, kwa sababu pambo hilo lilikuwa na chachu. Majiko ya umeme yalikuwa yakiwashwa ili kuangamiza chachu yoyote humo. Sahani maalum yaliyotumika katika sikukuu maalum walikuwa hawatunzi; sahani zilizotumika mara kwa mara zilibebwa na kuondolewa kwenye nyumba hadi Pasaka ilipokwisha. Maji yaliyokuwemo kwenye nyumba yalimwagwa nje na maji safi yaliletwa kutoka katika kisima na kuwekwa katika chombo kipya na kufunikwa ili kuzuia uchafu.

Chachu yote iliyokusanywa katika nyumba ilitolewa nje na tayari kwa ajili ya kuchoma asubuhi ya kuamkia Pasaka.

Baada ya nyumba kusafishwa kabisa, na siku kabla ya Pasaka, mama wa nyumbani anakabidhi nyumba kwa mkuu wa familia kwa ajili ya ukaguzi. Naye huenda kuzunguka nyumba nzima kutafuta na kukagua wakati msadizi mwingine wa kaya ana mshumaa akimulika ili kusaidia katika utafutaji wa chachu. Kabla ya kuanza utafutaji husema yafuatayo,"Heri Wewe, Ee Yehova, Mungu wetu, Mfalme wa Ulimwengu, unayetutakasa na amri zako na umetuamuru kuondoa chachu."

Wakati mkuu wa kaya hufanya kazi yake, kunakuwa na ukimya mkali kwa wengine wa kaya. Hakuna hata mmoja anayeruhusiwa kusema neno. Kama akipata chachu yoyote huondolewa kutoka ndani ya nyumba na kuwekwa pamoja na chachu iliyokusanywa hapo awali.

Utafutaji wake ukikamilika na isipopatikana chachu yoyote husema maneno haya, "Kila aina ya chachu ambayo ipo katika milki yangu ambayo Sijaona, ihesabiwe tupu, na kuonekana kama mavumbi ya nchi."

Muda wa saa nne asubuhi kabla ya Pasaka, chachu yote waliyokusanya huchomwa moto na Maombi yafuatayo husemwa: "Aina yoyote ya chachu ambayo ipo katika milki yangu, ambayo mimi nimeondoa, na aina yoyote ya chachu ambayo Sijaona na sikuondoa, itakuwa batili na ihesabiwe kuwa kama tupu na kuhesabiwa kama mavumbi ya nchi." Hii inaitwa"Beur Chametz,"au "maangamizi ya chachu." Wako huru toka dhambi na wako tayari kushirika sikukuuya mikate isiyotiwa chachu.

Paulo alijua Wayahudi watamuelewa pale aliposema katika 1 Kor. 5:7-8, "*Basi ondoeni chachu ya kale Jitakaseni, mkatupe mbali chachu, mpate kuwa donge jipya, kama hamkutiwa chachu. Maana, Pasaka wetu ni Kristo ametolewa sadaka kwa ajili yetu; Basi, natufanye karamu hiyo si kwa chachu ile ya kale, chachu ya ubaya na uovu, lakini pamoja na mkate usiotiwa chachu ya usafi na kweli*."

Chachu inatumika kama mfano wa dhambi, nyumba inawakilisha mioyo yetu ambayo lazima kutakaswa kutoka dhambini.

Pasaka ilikuwa ni sikukuu ya nyumbani, Si ya Umma

Kwa sehemu kubwa, Wayahudi walisheherekea sherehe zao za kidini katika sunagogi na kila mtu akiwa ameudhuria. Pasaka ilikuwa tofauti; ilikuwa inasheherekewa kama sikukuu ya nyumbani na watu wachache waliyoudhuria.

Idadi ya chini ya watu waliohudhuria sikukuu ya Pasaka ilikuwa 10 na kamwe wasizidi watu 20. Hakuna watu wa mataifa waliyoruhusiwa. Ni tofauti sana leo kuliko ilivyokuwa wakati wa Kristo. Sasa, wageni wasio Wayahudi walioalikwa kushiriki tukio la Pasaka walipangwa kwa masinagogi. Kitabu cha Wayahudi kiitwacho Talmud kiliweka idadi 10-20 ya wale wanaohudhuria.

Exo. 12:3-4, "*Semeni na makutano wote wa Israeli, Katika siku ya kumi ya mwezi huu watamtwaa mwana-kondoo wa kila mji , kulingana na nyumba za baba zao, mwana kondoo kwa ajili ya nyumba: Na kama kaya ina idadi ndogo mno kwa mwana-kondoo, basi yeye na jirani yake aliye karibu nyumbani kwake waungane kulingana na idadi ya watu; kila mtu kama ulaji wake ndivyo mtakavyofanya hesabu yenu kwa ajili ya kondoo*".

Walipaswa kuhakikisha kuwa si wachache sana waliyoweza kumla kondoo wasimmalize na pia wasiwe wengi sana wakuweza kuzuia kondoo asiwatosheleze.

Meza ya Pasaka

Meza lilikuwa linafunikwa na kitambaa safi ya kitani ambayo nguzo ya kusimamisha mishumaa na vyombo vya mishumaa viliwekwajuu yake. Katika sahani tofauti tofauti ziliwekwa makala yafuatayo: mikate isiyotiwa chachu imefungwa leso maalum, bakuli la mboga chung, sahani ya maji chumvi, mayai mawili yaliyochemshwa, apple lililo pasuliwa (baadhi ya kete waliweka vyombo vidogo dogo), kondoo aliyechomwa, na vikombe vinne vya matunda ya mzabibu kikundi cha Wayahudi wanaojaribu kuchunguza Pasaka kama ilivyoagizwa katika Talmud, wengine wana vikombe vinne tofauti wakati wengine wana magudulia makubwa na kutumia kikombe kimoja tu kwa ajili ya matukio yote manne).

Unaweza kutambua mambo yalio orodheshwa hapa ambayo hayakutajwa katika Agano la Kale.

Nataka kufafanua kwamba Wayahudi wanasema kuwa Musa akawapa Sheria ya mdomo ambayo ilitenganishwa kupitia miongo yote na mababu wa Kiyahudi. Hii hatimaye iliwekwa katika mfumo wa maandishi iitwayo Talmud (pia huitwa Mishna) karne nyingi kabla ya wakati wa Kristo.

Madhumuni halisi ya Talmud ilikuwa kufafanua zaidi maelezo ya desturi za dini ya Kiyahudi. Kwa mfano, Musa akawaambia wana wa Israeli walipaswa kula mboga chungu katika mlo wa Pasaka. Kilicho baki kwa hilo, kunaweza kukawa na maoni tofauti ya kitu gani kilicho elezewa kuwa ni mboga chungu. Hivyo kuwa thabiti Talmud inaelezea kuwa parsley, hisopo, na horseradish vitumike kwa ajili ya mboga uchungu. Talmud pia inazungumzia mengine mengi ya kidini mila na desturi.

Josephus (mwanahistoria wa Kiyahudi wakati wa Kristo) alifanya kumbukumbu ya Talmud, "Mafarisayo waliwapa watu kanuni fulani Fulani vilivyokabidhiwa na vizazi vya zamani na hazikuandikwa katika sheria za Musa". Josephus aliandika zaidi kuhusu vita ya Wayahudi lakini pia alikiri uwepo wa Kristo wakati wa maisha yake katika historia ya kitabu chake.

Sehemu mbalimbali katika Talmud iliitwa mpangilio iliyokuwa imegawanyika katika sehemu inayoitwa Tractates ambayo kulikuwa na 63 kwa idadi. Tractate 14 inaongelea maelekezo yao na sheria kuhusu Pasaka:

1. Kwa ajili ya kutafuta chachu.

2. Taka za chachu.

3. Keki ya pasaka na mboga chungu.

4. Kazi ya kufanya kabla ya Pasaka.

5. Mauaji ya kondoo wa Pasaka.

6. Kazi ya pasaka ni zaidi vizuizi vya Sabato.

7. Kupika Pasaka.

8. Watu waliyoruhusiwa kushiriki Pasaka.

9. Watu ambao hawakuruhusiwa kushiriki Pasaka.

10. Mazingira yasiyo ya kawaida.

11. Mpangilio wa kula Pasaka.

Talmud ilikuwa ikisemwa kwa mdomo na mababu wa Kiyahudi kisha kuweka katika mfumo wa maandishi miaka 584 kabla ya Kristo. Kumekuwa na baadhi ya matoleo tofauti au mbinu iliyoanzishwa tangu wakati huo:

1. Bavli version - Kuhusu 499 AD na wasomi wa Kiyahudi. Baadhi ya Tractates halisi yaliondolewa.

2. Pilpal – Iliundwa katika karne ya 15 na 16 katika Poland na Lithuania. Matumizi yake yalikoma katika Karne ya 18.

3. Sephardic – Ilitengenezwa katika karne ya 15 na kutumika awali na jumuiya za Kihispania na Italia. Ni bado maarufu leo na makundi mengi ya Wayahudi, hata hivyo desturi ya Pasaka ilikuwa tofauti katika hii toleo ikilinganishwa na ile ya wakati wa Kristo.

4. Critical - Iliundwa katika karne ya 19.

5. Brisker – iliundwa katika karne ya 19

6. Jumuiya ya Wayahudi wa Kiorthodox wanachunguza Pasaka mara nyingi kwa karibu Talmud halisi ya Kiyahudi. Hivyo kama ukizungumza na Myahudi leo na kutaka kujua kuhusu mila zao, ni muhimu kujua ni jumuiya ipi ya Kiyahudi anayotoka.

Maelekezo Kuhusu Pasaka

Katika mwanzo wa Pasaka kawaida mama wa nyumba huwasha mishumaa mezani. Mwana familia yeyote wa Kiyahudi hukaribishwa.

Wana familia walikuwa wanavaa nguo zao nzuri za kusafiria na viatu katika miguu yao kana kwamba walikuwa wanakwenda katika safari ya haraka, kama ilivyokuwa wakati wakikimbia kutoka Misri na Musa.

Mkate ulitengenezwa na unga usiyo chachwa. Ilikuwa hairuhusiwi kukaa muda, lakini ilikuwa inaokwa mara moja kwa kuzuia kuumuka.

Kuna kutokuelewana leo kati ya washiriki wa Kanisa kwamba ni vifungu vipi vinavyopaswa kutumika katika kutengeneza mkate usiochachu. Baadhi wana nukuu baadhi ya kifungu cha Agano la Kale wakati wengine wananukuu kifungu kingine ambacho kina maagizo tofauti kuhusu kutengeneza mkate usiyo chachwa. Ni muhimu kufahamu kwamba maandalizi ya mikate isiyotiwa chachu ilitegemea na dini ipi ambayo ingelitumika.

1. Katika kuwaweka wakifu makuhani (Kut. 29 na Mambo ya Walaw 7.), Mikate isiyotiwa chachu ilikuwa inatengenezwa na mafuta.

2. Katika sadaka za nyama (Lawi 2 na Lawi 6.), Mikate isiyotiwa chachu ilikuwa inatengenezwa na mafuta na ubani na kuchanganywa na chumvi.

3. Katika sadaka ya hatia (Law 5), mikate isiyotiwa chachu ilikuwa inatengenezwa bila mafuta au ubani.

4. Katika Pasaka (Kut. 12 na Law 23), ni mkate usiotiwa chachu ndiyo imetajwa; mafuta na ubani havikutajwa. Katika tovuti ya Kiyahudi ya wa Orthodox ilikusudiwa kwa ajili ya waumini wa Kiyahudi, kulikuwa na mkazo kwamba mafuta na ubani visitumike katika mkate usiotiwa chachu wakati wa Pasaka. Hii anakubaliana na maandiko ya kale ya Wayahudi juu ya matengenezo ya mikate isiyotiwa chachu kwa ajili ya Pasaka kwamba ni unga na maji tu ndiyo yangetumika.

Kulikuwa na mikate mitatu isiyotiwa chachu iliyo unganishwa pamoja mezani. Ukimuuliza leo Myahudi mikate mitatu iliwakisha nini, baadhi watasema, "ya juu ni ukuhani, ya katikati ni Walawi, na ya chini ni ya wa Israeli wote." Kwa wakati mmoja yalimuwakilisha Mungu, Kristo, na Roho Mtakatifu. Kwa sababu ya karaha ya Wayahudi kwa ajili ya Kristo kuwa anajulikana kama Masihi, hawa Wayahudi walibadilisha maana ya mikate.

Ibada ya Pasaka, kiongozi wa familia aliweka mkate wa kati(ile iliyo muwakilisha Masihi) chini ya mto kana kwamba anaificha. Maana yake ilikuwa kwamba ifichwe au izikwe, akionyesha kifo, kuzikwa, na kufufuka kwa Masihi kama ilivyo tabiriwa. Mkate huu uliyofichwa uliitwa Aphikomen, ikimaanisha "manna iliyofichwa". Baadaye, baada ya maombi ilitolewa kutoka chini ya mto, kuvunjwa vipande viwili, kipande kimoja kilipitishwa kwa wanafamilia kwa ajili ya kula. Kipande kingine iliwekwa kwenye sahani iliyokuwa tupu iliyowekwa akiba kwa ajili ya Eliyah au Masihi. Hii ilitendeka kwa karne nyingi kabla ya kuja kwa Kristo. Leo hii, wengi hufanya mchezo wa kuficha mana na watoto. Wanatumwa nje ya nyumba, mana inafichwa mahali fulani katika chumba, na watoto huitwa ndani ili kuitafuta mana.

Zoezi la kuficha mana ili zungumziwa katika Ufunuo 2:17, "... *Wale wanaoshinda mimi nitawapa ile mana iliyofichika,* ..."

Mikate mingine miwili walikula wakati wa Pasaka.

Tunapo kula mkate uliyovunjwa katika meza ya Bwana tunaitangaza mauti ya Bwana, mpaka atakapokuja. 1 Kor. 11:26, "*Kwa maana mkila mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana, hata ajapo.*"mwili wa Yesu uliyo vunjika ulitimiza mkate ule wa katika kwaajili yetu.

Mboga chungu na Maji ya Chumvi

Wayahudi walikuwa na mboga chungu katika meza ya pasaka kulingana na Kut.12:8, "*Na Watakula nyama usiku huo, iliyochomwa moto, na mikate isiyochachwa; tena pamoja na mboga zenye uchungu watakula.*"

Mayai ya kuchemsha na maji ya chumvi hazikutajwa katika Agano la Kale lakini yametajwa katika Talmud ambayo inazunguzia kwa kina sheria zote na maelekezo kwa ajili ya huduma hii, pamoja na mengine. Talmud inachukuliwa na Wayahudi kuwa sheria na takatifu.

Sasa,Talmud haina maana? Hapana ilianza kwa kufafanua mila na desturi zao. Baadaye, Wayahudi waliichukulia kama sheria. Wayahudi walimtuhumu Yesu kwa kutotii kile kilichoandikwa katika Talmud. (Katika kifuatacho baadhi ya Tafsiri husema ngano; wengine wanasema nafaka).

Luka 6:1-5, " *Ikawa siku ya sabato moja, alikuwa akipita katika mashamba wanafunzi wake wakawa wakivunja masuke na kuyala, wakiyapukusa –pukusa mikononi mwao. Basi baadhi ya Mafarisayo wakawaambia, Mbona mnafanya lisilo halali siku ya Sabato? Yesu akawajibu, akawaambia, hamkulisoma hata hilo alilolifanya Daudi alipokuwa na njaa, yeye na wale aliokuwa nao? Jinsi alivyoingia katika nyumba ya Mungu, akaitwaa mikate ile ya wonyesho, akaila akawapa na hao wenziwe, ambayo si halali kuila ila kwa makuhani peke yao. Akawaambia, Mwana wa Adam ndiye Bwana wa Sabato.*" **<u>Baadhi ya tafsiri husema "ngano" zingine husema "masuke"</u>**

Sheria ambayo Mafarisayo walifahamu ilikuwa katika Talmud, siyo sheria ya Musa. Talmud ilikuwa tofauti na kile Musa alicho waambia katika Kumb. 23:25, kuhusu kula siku ya Sabato, "*Uingiapo katika mmea wa jirani yako, waweza kuyapurura masuke kwa mkono wako, ila usisogeze mundu katika mmea wa jirani yako.*"

Kwa mujibu wa sheria ya Musa Yesu hakufanya chochote kibaya. Wayahudi waligeuza desturi yaTalmud kuwa sheria yao. Wakati mwingine desturi hizi zilipingana na sheria ya Musa.

Matt. 15:1-3, "*Ndipo mafarisayo na waandishi toka Yerusalemu walipomwendea Yesu wakisema, mbona wanafunzi wako huyaalifu mapokeo ya wazee, kwa maana hawanawi mikono walapo chakula. Akajibu akawaambia, mbona ninyi nanyi huihalifu amri ya Mungu kwaajili ya mapokeo yenu?*"

Wakati wowote unapoona neno katika Biblia, "*mapokeo ya wazee*", inamaanisha Talmud.

Je, Yesu alikataa yote ya Talmud? Hapana. Baadhi ya vitu alivyotumia katika Pasaka vilitajwa katika Talmud. Kile alichokataa ni mambo yaliyokuwa katika Talmud yaliyopingana na sheria ya Musa.

Kila Myahudi alikuwa akila kipande cha mboga chungu (horseradish, iliki, na hisopo) na mayai mawili ambayo yalimkumbusha maisha ya uchungu ya wazazi wake wakiishi katika utumwa. Hii walichovya katika bakuli la maji ya chumvi wao huita"*sop*". Sop kwa Myahudi kilikuwa ni kitu ambacho chakula ilikuwa ikichoviwamo; inaweza kuwa supu, mchuzi, au kimiminio yoyote. Matumizi yaliyozoeleka ya sop katika milo mingine ilikuwa ni kuchovya mkate uliyo chachwa katika supu na kula. Mkate uliyo chachwa haikuruhusiwa wakati wa Pasaka, kwa hiyo haikuwa kusudi la sop kwa muda huo. Sop iliyotumika katika Pasaka ilikuwa ya maji ya chumvi.Mboga chungu na mayai wawili yalichovya katika sop (Maji ya chumvi) kwa mikono na kuliwa; hii iliwakumbusha macho na machozi ya baba zao.

Yesu alifanya hivyo wakati wa maadhimisho ya Pasaka yake. Matt.26:23, "*Akajibu akasema, Yeye aliyetia mkono wake pamoja nami katika kombe, ndiye atakae nisaliti.*"

Yohana 13:21-27, "*Naye alipokwisha kusema hayo, Yesu alifadhaika rohoni, akashuhudia akisema, Amin, amin, nawambieni, mmoja wenu atanisaliti. Wanafunzi wakatazamana huku wakiona shaka ni nani amtajaye. Na palikuwapo mmoja wa wanafunzi wake, ameegama kifuani pa Yesu ambaye Yesu alimpenda……*"

Sop kamwe haikutumika kunawia kama leo baadhi ya watu wanavyoamini, bali ilitumika kama sehemu ya mlo. Sop inaweza kuwa kimiminio, mchuzi au supu ambayo mtu anachovya chakula chake kabla ya

kula. Sop ya Pasaka mara zote ilikuwa ni maji ya chumvi ambayo walichovya mboga chungu na mayai mara mbili kabla ya kula.

Katika hili, tunaona hapa kuwa Yesu alisherehekea sikuu za Pasaka kama ilivyoandikwa katika Talmud. Yuda alichovya mkono wake na Bwana katika bakuli na akaenda nje**. Pia kumbuka wale waliyo kuwepo katika Pasaka hii walikuwa wanaegama upande walipokuwa wakila**. **Yuda** hakuwepo wakati Yesu alianzisha meza ya Bwana.

Epo iliyokatwa

Tena, hitaji hili halikuwa katika Biblia, lakini lilikuwa katika Talmud, na ilikuwa ikitiliwa maanani na Wayahudi. Mkuu wa familia alikata tunda hili vipande vipande kwa mfumo wa mraba(kila aliye udhuria alipewa kipande kimoja kimoja) ikiwakumbusha Wayahudi chokaa na matofali ambayo baba zao walikuwa wakitengeneza ili kujenga miji ya Farao. Kila mtu alitakiwa kula kipande mraba.

Mwanakondoo wa Pasaka

Kulingana na Exo. 12:1-5, kulikuwa na mwana-kondoo kwenye meza ya Pasaka. Kondoo huyo alikuwa bila doa au kilema na alikuwa anachaguliwa katika siku ya 10 ya mwezi wa Nisani, au siku 5 kabla ya Pasaka. Exo. 12:1-5, "*Na Bwana akasema na Musa na Haruni katika nchi ya Misri akisema, Mwezi huu utakuwa mwanzo kwenu ya miezi utakuwa ni mwezi wa kwanza wa mwaka kwenu. Semeni na kwa mkutano wote wa Israeli, akisema, Katika siku ya kumi ya mwezi huu atatwaa kila mtu mwana-kondoo, kwa hesabu ya nyumba zao baba, mwana-kondoo kwa nyumba: Na kama kaya kuwa kidogo mno kwa mwana-kondoo, basi yeye na jirani yake aliye karibu nyumbani kwake kuchukua kulingana na idadi ya watu; kila mtu kama ulaji wake atafanya hesabu yenu kwa mwana-kondoo. Kondoo wenu atakuwa hana ila, mume wa mwaka wa kwanza: nanyi kuchukua nje katika kondoo au katika mbuzi:*"

Ilipaswa kuwa mzaliwa wa kwanza; ilikuwa ikichomwa moto; na mfupa wake haukuvunjwa. Maumivu makubwa yalifanyika ili kuhakikisha inakuwa hivyo. Ingeweza kuuawa na kuchomwa, na kuliwa yote wakati wa jioni ya tarehe 14 ya mwezi wa Nisani. Exo. 12:8-10, "*Watakula nyama yake usiku ule, kuchoma moto, na mikate isiyochachwa; na kwa mboga zenye uchungu yake. Msiile mbichi, wala ya kutokoswa majini,bali uta okwa motoni; kichwa chake pamoja na miguu yake, na nyama zake za ndani. Nanyi basi chochote, na hicho kitakachosalia hata asubuhi mtakichoma kwa moto.*"

Ni jinsi gani nyakati zimebadilika. Leo hii wanachukua kondoo mbaya (si kondoo mzima) katika bucha kwa kawaida siku moja kabla, lakini baadhi wanaruhusu inunuliwe wakati mwingine wiki moja kabla.

Inawezaje kuthibitishwa na mkuu wa familia binafsi kwamba ilikuwa haina doa au kilema na je alikuwa kondoo mzaliwa wa kwanza? Kuwa tu kiweo mfupa inaweza kuwa haikuvunjwa, lakini ilitenganishwa na sehemu zingine za mwili.

Rafiki yangu mpendwa wa kanisa la Kristo aliniambia kuwa yeye na mkewe walialikwa kula pasaka na marafiki zao wa kiyahudi. Badala ya mwanakondoo walitengewa nyama ya kuku, KUKU!? Kulikuwa na matatizo mawili hapa:

1. Ilikuwa ni kinyume na sheria ya Musa kwa mtu yeyote ambaye hakuwa muyahudi kula Pasaka

2. Wayahudi waliamriwa kuandaa mwana kondoo, siyo kuku. Je, hawata jifunza?

Yesu ni Mwana-kondoo wetu asiye na doa aliyetolewa kwamba alikuwa sadaka na hakuna mfupa wa mwili wake uliyovunjika.

Yohana 1:29, "*Siku ya pili, Yohane alimwona Yesu akimjia, akasema, Tazama Mwana kondoo wa Mungu aondoaye dhambi ya ulimwengu.*"

Yohana 19:31-36, "*Wayahudi, kwa sababu ni Maandalio, miili haipaswi kubaki juu ya misalaba siku ya Sabato (kwa kuwa siku ya Sabato ilikuwa siku kubwa), alimwomba Pilato ruhusa ya miguu yao ili*

ivunjwe na kwamba miili yao iondolewe. Basi, askari walikwenda, wakaivunja miguu wa kwanza na wa pili, aliyesulibiwa pamoja Yesu. Lakini walipomfikia Yesu waliona kwamba amekwisha kufa, na hivyo hawakumvunja miguu yake: Lakini askari mmoja alimtoboa ubavuni kwa mkuki, na mara ikatoka damu na maji. Naye aliyeona ameshuhudia, na ushuhuda wake ni kweli: na yeye anajua ya kuwa anasema kweli ili ninyi nanyi mpate kusadiki. Kwa maana hayo yalitukia ili andiko kutimia, Hapana mfupa wake utakaovunjwa."

Mifupa ya Kristo haikuvunjwa, lakini mwili wake ulivunjwa. Zakaria. 12:10, "*Nami nitawamwagia watu wa nyumba ya Daudi, na wenyeji wa Yerusalemu, roho ya neema na kuomba; nao watamtazama juu yangu waliyemtoboa, nao wataomboleza kwa ajili yake, kama moja inaomboleza kwa ajili ya mwana wake wa pekee, na uchungu kwa ajili yake, kama mtu ni uchungu kwa ajili ya mzaliwa wake wa kwanza.*"

Yohana 19:34, "*Lakini askari mmoja alimtoboa ubavuni kwa mkuki, na mara ikatoka damu na maji.*"

Baadhi ya makanisa ya Kristo hudai kwamba hatupaswi kuvunja mkate kwa sababu mifupa ya Kristo haikuvunjwa. Nitaongelea hili katika sehem ya pili la (2)somo hili.

Kikombe

Kwa mujibu wa Sheria ya Pasaka kulipawsa kuwa na vikombe 4 vya mzao wa mzabibu juu ya meza. Hakuna mtu aliyekuwa na kikombe chake wenyewe. Kulikuwa na vikombe 4 tofauti vilivyotumika au kikombe kimoja tu kilitumika, lakini kujazwa kwa nyakati nne tofauti wakati wa Pasaka (kulingana na kundi la Wayahudi waliyoshiriki Pasaka). Katika hatua yoyote wote walinywea kikombe kimoja ya tukio hilo kila wakati wa Pasaka.

Juisi ya zabibu tu ilitumika kama chachu yote ingeweza kuondolewa kutoka ndani.

Pia, Talmud ilieleza kuwa kinywaji iliyopaswa kutumika katika Pasaka kuwa ni juisi ambayo haiku changanywa. Kwani hakuna chachu ilikuwa inaruhusiwa wakati wa Pasaka, ilikuwa na maana maji ya zabibu ambayo ingetumika haikuchanganywa.

Kunywa uzao wa mzabibu iliwakumbusha damu ya Mwanakondoo iliyopakwa kwenye miimo ya mlango na juu ya mlango ili pigo la malaika wa mauti aweze kupita juu ya mababu zao. Exo. 12:13, "*Na damu itakuwa kwenu ni ishara na wakati mimi nitaona damu, mimi nitapita juu yenu, lisiwapate pigo hautakuwa juu wewe kuwaangamiza, wakati mimi kuipiga nchi ya Misri.*"

Kwa nini vikombe vinne? Kila kikombe kilibebwa kwa nyakati nne tofauti wakati wa Pasaka; Vitatu vilinyweka na washiriki, cha nne kiliwekwa akiba kwa ajili ya Eliya au Masihi.

Kikombe cha kwanza ni Kiddush, ambayo ina maana ya utakaso.

Kikombe cha pili inaitwa kikombe cha mapigo.

Kikombe ya tatu inaitwa kikombe ya ukombozi.

Kikombe cha nne ni mara nyingi huitwa hallel ambayo ina maana ya sifa. Wakati mwingine inaitwa kikombe cha kukubalika, au kikombe cha Eliya. Pia inaitwa kikombe cha baraka. Paulo anazungumzia kikombe ambacho Yesu alitumia alipoanzisha meza ya Bwana alikiita kikombe cha baraka. Baadhi ya makundi ya Wayahudi leo huita kikombe cha tatu "*kikombe cha baraka*" na wanakinywea badala ya kuweka kwenye sahani akiba kwa ajili ya Masihi, kama ilivyokuwa desturi wakati wa Kristo.

Mkuu wa nyumba anatwaa kikombe cha kwanza, akashukuru, akanywa kidogo, na kupitishwa kwa wengine, ambao wote walikunywa kidogo.

Kila mmoja alikula mboga chungu na hesabu ya Pasaka ya malaika wa kifo kusoma kwa sauti.

Mtu mwenye umri mdogo aliuliza, "Kwa nini usiku huu tofauti na siku nyingine zote?"

Mkuu wa nyumba basi alielezea maana yake na kuishia na, "Katika umri kila mtu ana wajibu wa kutambua mwenyewe kuwa ametoka nje ya Misri ... Ni kwa sababu ya yale Bwana aliyonifanyia nilipotokanje ya Misri".

Wakati wa Pasaka mtoto pia anauliza maswali yafuatayo kisha mkuu wa kaya anajibu:

1. Ni kwanini katika siku zingine hatuchovyi chakula yetu hata mara moja, lakini katika usiku huu tunachovya mara mbili?

2. Ni kwa nini, katika usiku nyingine sisi zote tunakula mkate uliyochachwa, lakini katika usiku tunakula matza (mkate usiyo chachwa)?

3. Ni kwa nini usiku zingine tunakula kila aina ya mboga mboga, lakini katika usiku huu sisi hula mboga za chungu?

4. Ni kwa nini siku zingine zote tunakula tukiwa tumekaa wima au wakilala, lakini katika usiku huu sisi wote tumeegemea? Ni meza bila miguu. Walikuwa kuchunguza Pasaka katika namna ile ile kama walivyofanya baba zao, katika Pasaka ya awali, ambayo ilimaanisha milki yao binafsi na kuwa tayari kwa ajili ya kusafiri, hakuna meza iliyo kuwa na miguu. meza ya Pasaka ilikuwa sanda ya kitani iliyotandikwa kwenye sakafu.

Kikombe cha pili kilibarikiwa, akanywa kidogo, na ikapitishwa kwa watu wengine, ambao wote walikunywa humo.

Kisha Zaburi 113 na 114 iliimbwa.

Kisha chakula kililiwa, ikiwa ni pamoja na kondoo wa kuchoma.

Kikombe cha tatu alibariki kisha, akanywa kidogo, na kupitishwa kwa wengine kunywa.

Mikate ile miwili ililiwa na chakula.

Ilikuwa baada ya kikombe cha tatu ndipo mkuu wa familia alichukua mkate usiotiwa chachu kutoka chini ya mto, aliuliza baraka ya Mungu juu yake, akaumega nusu na nusu nyingine akaweka katika sahani ya wazi kwaajili ya Masihi.

Kikombe cha nne daima kiliwekwa pamoja na sahani tupu ambayo ilikuwa akiba kwa ajili ya Masihi (baadhi ya kumbukumbu yanasema Eliya). Baadhi wanaamini kwamba Eliya atarudi kabla ya Masihi.

Kikombe hii iliitwa "*kikombe cha baraka*". Paulo alizungumzia kikombe hiki cha nne pale Yesu alipoanzisha meza yake.

1 Kor. 10:16, "*Kikombe kile cha baraka tukibarikicho, si ushirika wa damu ya Kristo? Na tunapoumega mkate, je, huwa hatushiriki mwili wa Kristo?*"

Nawaulizeni, je, ni wapi katika Agano la Kale neno "*kikombe cha baraka*" kimetumika? Unaweza kutafuta utakavyo, haipatikani popote pale katika Bibli. Hapana, neno "*kikombe cha baraka*" haipatikani katika Biblia lakini ilitajwa katika Talmud kama ile akiba kwa ajili ya Masihi.

Kichwa cha familia basi anatoa wito wafungue mlango, "Wewe Mungu wa Abrahamu, Isaka na Yakobo, kwa muda mrefu tumesubiri ahadi yako. Tunakuomba sasa, umtume mpakwa mafuta wako uliyeahidi, Mwana wa Daudi. Kuwa na huruma juu ya watu wako Israeli. Tukusanye kulingana na neno lako na tutakuwa watu wako na Wewe utakuwa furaha ndani yetu kama ya zamani. Tazama mambo yote tayari na sisi tunasubiri."

Kisha anasema kwa sauti kubwa, "Ibarikiwe kuingia kwa Mesiah au Eliya na baada ya kusubiri kwa mda mfupi mlango unafungwa "

Baada ya dakika chache ya kusubiri mlango unafungwa.

Mkuu wa familia anafanya maombi zaidi kwa Mungu, "Kwa muda gani tutakuwa tunasubiri, Bwana!" (toleo limefupishwa ya kile alichosema).

Pasaka ilihitimishwa kwa kusoma Zaburi 115-118 na kuimba Zaburi 136.

Yesu na wanafunzi wake waliimba wimbo baada ya kuanzisha meza ya Yake. Matt. 26:30, "*Na Baada ya kuimba wimbo, wakaondoka, wakaenda katika mlima wa Mizeituni.*"

Makala hii inaendelea katika sehemu ya 2 ya "*Pasaka na meza ya Bwana.*"

29 Michelson, op. cit., uk. 20

30 Michelson, loc. cit.

Bibliografia

- Mwandishi Hajulikani, Sabato Kuu", Wikipedia – The Free Encyclopedia, August 4, 2011.
- Mwandishi Hajulikani, "Pasaka ya Kiyahudi", Wikipedia – The Free Encyclopedia, Septemba 2, 2010.
- Mwandishi Hajulikani, "Talmud", Wikipedia – The Free Encyclopedia, March 2, 2012.
- Mwandishi Hajulikani, "Verse Search", Mfumo wa Utafiti wa Biblia, Austin, Texas, 2005.
- Brickner, David, "Maajabu ya Kikombe cha Pasaka", jewsforjesus.org/publication/newsletter/2002_03/mystery website.
- Coffman, James Burton, Commentary on Mark, A. C. U. Press, Abilene, TX, 1975
- LaSor, William Sanford, Daily life in Bible Times, Standard Publishing, Cincinnati, Ohio, 1996
- Michelson, Arthur U., The Jewish Passover And the Lord's Supper, The Jewish Hope Publishing House, Los Angels, CA, 1936.
- White, Jr., W., "Talmud", The Zondervan Pictorial Encyclopedia of Bible, Vol 5, Regency Library, Zondervan Publishing house, Grand Rapids, Michigan, 1976.